



Idara ya Elimu ya NSW

## Kutuma ombi kwa mtoto wangu kuhudhuria darasa la fursa au shule ya elimu ya juu ya kuchagua

### Kwa nini elimu ya kuchagua?

Kuweka pamoja wanafunzi wenye uwezo wa juu na wenye vipawa katika kikundi na kutumia mbinu maalum za kufundishia huwasaidia:

- ukuaji wao wa kitaaluma
- ustawi wao wa kihisia; na
- urafiki wao na maisha yao ya kijamii.

Wanafunzi hutuambia kuwa wanapenda kujifunza zaidi wakati wenzao darasani wanapokuwa na uwezo na maslahi sawa.

### Je, ni sawa kwa mtoto wangu?

Hapa kuna alama kadhaa kuwa mtoto wako anaweza kupata faida kutoka elimu ya kuchagua.



anajifunza haraka na kwa rahisi



ana motisha ya juu



huuliza maswali magumu



ana kumbukumbu nzuri



mwenye mdadisi na mbunifu



huchunguza kwa undani masilahi

Kumbuka, uwezo wa juu wa watoto wengine wanaweza kufichwa. Kuwa katika darasa la fursa au shule ya juu ya kuchagua inaweza kusaidia.

# Je, ninaweza kumsaidia mtoto wangu kupitia mchakato wa kutuma ombi?



Zungumza na mtoto wako kuhusu **faida** na **changamoto** za elimu ya kuchagua na kushughulikia maswali na masuala yao.



Muulize **mwalimu wa mtoto** wako (au wafanyakazi wengine unaomfahamu vizuri) kama anafikiri elimu ya kuchagua itamfaa mtoto wako.



Omba **marekebisho** yoyote **yanayohitajika** kwa ulemavu au hali ya matibabu.



Mhimize mtoto wako kutumia **rasilimali za bure** za idara ili kujiandaa kwa ajili ya mtihani.



Kumbusha mtoto wako anahitaji tu kufanya **kiasi kidogo cha maandalizi** kwa mtihani ya uwekaji, na haitaji kufundishwa.



Umsaidie mtoto wako kuendelea na **shughuli ziada za mtaala**, kuwaona marafiki, kula kwa afya na kulala vizuri kabla ya kufanya mtihani.

**Mfano wa Upangaji Usawa** huhifadhi hadi **20% ya nafasi** katika madarasa ya fursa na shule ya juu ya kuchagua kwa wanafunzi wenye uwezo wa juu na wenye vipawa na:

- kutoka asili ya chini ya faida ya kijamii na kielimu
- wanafunzi wa Asili (Aboriginal) na/au wa visiwa wa Torres Strait
- kutoka vijijini na maeneo ya mbali
- wenye ulemavu.

Jifunze zaidi:

[edu.nsw.link/equity](https://edu.nsw.link/equity)

<https://education.nsw.gov.au/public-schools/selective-high-schools-and-opportunity-classes/general-information/translated-resources>



## Usaidizi wa kifedha

[edu.nsw.link/pubedu](https://edu.nsw.link/pubedu)

[Public Education Foundation scholarships](#) (ruzuku za masomo za Mfuko wa Elimu ya Umma) hutoa usaidizi wa kifedha ili kuwasaidia vijana katika shule za umma za NSW ili kupata fursa na kufikia uwezo wao.

*Tafadhali kumbuka kwamba hakuna ada ya kutuma ombi na kufanya mtihani wa upangaji, na hakuna ada za shule ili kujiandikisha katika shule ya juu ya kuchagua au darasa la fursa.*

## Uwe tayari ya kutuma ombi

Jifunze zaidi kwenye tovuti yetu



## Huduma ya mkaliani wa simu

Ikiwa unahitaji usaidizi wa mkalimani ili kuongea na mwalimu wa mtoto wako tafadhali piga simu kwa Hudumu ya Mkalimani wa Simu kwenye 131 450 na uliza kwa mkalimani katika lugha yako. Umwambie mwendeshaje simu ile nambari unayotaka kupiga simu, na mpigaji simu atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa kwa hududma hii.